

Tulipataje Chanjo za COVID-19 haraka sana?

Februari 23, 2021

Chini ya mwaka, tangu mwanzo wa janga la COVID-19, chanjo kadhaa tayari zimeshatengenezwa na kuidhinishwa. Taarifa hii inaelezea jinsi hii ilitokea haraka. **Habari katika taarifa hii imethibitishwa na madaktari na watafiti.**



1. Wanasayansi, serikali na mashirika ya kimataifa walikuwa wakijiandaa kiviipi kwa janga hii.

- Wanasayansi, serikali na mashirika ya kimataifa kutoka nchi tofauti wamekuwa wakitarajia janga kwa miaka mingi na tayari walikuwa wameunda ushirikiano ili kuharakisha mchakato wa kutengeneza chanjo.
- COVID-19 sio aina mpya kabisa ya virusi. Ni sawa na virusi vingine vya Korona kama virusi vya SARS, ambavyo vilikuwa vimechunguzwa kwa kirefu.
- Teknolojia ya mRNA ambayo imekuwa ikitumika kuzarisha chanjo mbili zinazopatikana Canada (Pfizer-BioNTech na Moderna) ilikuwa tayari imetengenezwa na kuchunguzwa kwa kuinga magonjwa mengine ya kuambukiza. Kwa hivyo teknolojia hii iliweza kutumika haraka sana mara tu virusi vya COVID-19 vilipogunduliwa.

2. Wahusika wote walikuwa wakishirikiana na kufanya kazi kwa ufanisi.

- Nyenzo za maumbile kutoka kwa virusi zilitambuliwa haraka sana na zikatangazwa wazi kwa umma.
- Kuongezeka kwa fedha za misaada kutoka ulimwengo wote, ili kusaidia kwa utafiti wa chanjo ya COVID-19.
- Majaribio na utafiti yalikuwa yakiendelea katika vituo mbali mbali ulimwenguni.
- Watafiti wanaojishughulisha na utayarishaji wa chanjo walitumia njia za elektroniki kukusanya na kushiriki data zao kwa njia fanisi.

3. Watu wengi walijitolea kupimwa.

Chanjo haziwezi kupitishwa mpaka zijaribiwe kwa idadi kubwa ya wanadamu. Majaribio haya huitwa "majaribio ya kliniki". Kulikuwa na msaada mkubwa wa umma kwa majaribio ya kliniki ya COVID-19 na maelfu ya watu wa asili zote walijitolea haraka kushiriki katika majaribio hayo. Kwa hivyo saizi wa majaribio ya kliniki ya kukuza chanjo za COVID-19 ilizidi ukubwa wa kawaida wa majaribio ya aina hii.

4. Viwango vya juu vya maambukizo vimesaidia jaribio la chanjo.

- Viwango vya juu vya maambukizo ya COVID-19 vilifanya iwe rahisi kuona ikiwa chanjo zinatoa kinga dhidi ya COVID-19. Baada ya mda mfupi, kulikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wanaouguwa COVID-19 katika kikundi ambacho hakikupokea chanjo hiyo, ikilinganishwa na kikundi kilichopokea chanjo hiyo. Hii ilionyesha kuwa chanjo hiyo ilikuwa na matokeo mazuri.
- Mara nyingi, watafiti wanapaswa kujaribu mara kadhaa kabla ya kuunda chanjo inayofaa. Lakini chanjo za kwanza za COVID-19 zilikuwa na matokeo mazuri wakati wa majaribio.

5. Taratibu za ukaguzi na udhibiti zilianza mapema.

Hapo zamani, serikali na baraza zingine za udhibiti hazikuanza michakato yao ya kukagua chanjo hadi baada ya utafiti na upimaji wao kukamilika. Lakini wakati huu, walikagua data ya utafiti katika kila hatua ya utafiti, hii ilifanya mchakato wa kukagua uwe na ufanisi zaidi. Hakuna hatua za usalama ambazo zilirukwa. Michakato ya kiutawala ilifanywa wakati huo huo na mchakato wa utafiti, jambo ambalo liliokoa wakati mwingi.



Tumebahatika sana kupata chanjo za COVID-19 zinazotayarishwa na kusambazwa ndani ya mwaka mmoja. Inatia moyo kujua kwamba hakuna michakato yoyote ya usalama ambayo ilirukwa katika utayarishaji wa chanjo ya COVID-19.

Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi chanjo zilivyoidhinishwa nchini Canada, tembelea ukurasa wa tovuti wa Health Canada hapa:

<https://www.canada.ca/en/public-health/services/diseases/2019-novel-coronavirus-infection/prevention-risks/covid-19-vaccine-treatment.html> (Kiingereza)

<https://www.canada.ca/fr/sante-publique/services/maladies/2019-nouveau-coronavirus/prevention-risques/covid-19-vaccins-traitements.html> (Kifaransa)

Habari katika taarifa hii imethibitishwa na madaktari wa Canada: Meb Rashid MD, Profesa Msaidizi, Chuo kikuu cha Toronto; Vanessa Redditt, MD, Mhadhiri, Chuo kikuu cha Toronto; na Isaac I. Bogoch, MD, Profesa Mshirika, Chuo kikuu cha Toronto

